Mkulima Mbunifu

Jarida la kilimo endelevu Afrika Mashariki

biovision

Toleo la 52, Januari 2017

Yaliyomo

Chaya 2

Uvunaji wa Samaki 4 & 5



Mfumo wa kufugia kuku 7

# Nane Nane: Wadau wa kilimo na ufugaji tujitokeze




Picha: MkM

Kama ilivyo desturi kila mwaka kuadhimishwa kwa sherehe za kilimo, uvuvi na ufugaji nchini Tanzania almaarufu kama "Nane Nane'', ni wazi kuwa mwaka huu pia maandalizi ya sherehe hizo zimeanza kupamba moto katika kila mkoa hapa nchini kupitia kwa waandaji TASO.

Kwa mwaka huu wa 2017, kauli mbiu katika sherehe hizo za Nane Nane zinazotegemewa kuanza mapema tarehe 1/8/2017 na kufikia kilele chake tarehe 8/8/2017 ni "ZALISHA KWA TIJA MAZAO NA BIDHAA ZA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI ILI KUFIKIA UCHUMI WA KATI''.

Mkulima Mbunifu kama mmoja wa wadau wa maonyesho hayo tunawakumbusha wakulima, wafugaji, wavuvi, na wadau wote kujitokeza na kushiriki kwa wingi na kikamilifu ili kunadi bidhaa zenu pamoja na kujifunza mengi kutoka kwa wadau mbalimbali na kukuza shughuli za kilimo na ufugaji.

Tukumbuke kuwa, sherehe hizi kila mwaka zinakuja na fursa mpya kwa wadau wote hivyo ni muhimu sana kushiriki ili kujifunza na kuona namna ya kuzalisha mazao na bidhaa mbalimbali kwa tija kwa lengo la kufikia uchumi wa kati utakaomnufaisha mkulima, mfugaji, mnunuzi na hata mlaji kama kauli mbiu inavyojieleza.

# Tambua mfumo sahihi wa kufugia

Mfugaji awaye yeyote, kabla ya kuanza mradi wa ufugaji wa kuku ni lazima kwanza akatambua ni mfumo gani au ni njia gani atatumia katika ufugaji ili kuweza kujipanga kwa ajili ya mahitaji na gharama za mfumo husika.

Kwa ujumla, njia rahisi na inayopendekezwa kutumiwa na mfugaji



Picha: MkM

wa kawaida kijijini ni ya ufugaji wa nusu ndani na nusu nje, yaani nusu huria.

Hii inatokana na faida zake kama zitakazoainishwa katika ukurasa wa 7. Kwa kutumia mfumo huu wa ufugaji, utaepuka hasara za kufuga kwa mtindo wa huria kama zitakavyofafanuliwa kwa undani katika jarida hili.

**MkM kwenye mtandao**

Njia ya mtandao yaani internet, inawasaidia wale wote ambao hawana namna ya kupata machapisho ya Mkulima Mbunifu moja kwa moja, kusoma kwenye mtandao na hata kupakua nakala zao wao wenyewe.

www.mkulimambunifu.org
https://issuu.com/mkulimambunifu
www.facebook.com/mkulimambunifu
www.twitter.com/mkulimambunifu
+255 785 496 036

## *Mpendwa Mkulima*

*Kwa miaka ya sasa, uzalishaji wa mazao ya kilimo na ufugaji kwa lengo la kuzalisha bidhaa kamili na si ghafi linakuwa kwa kasi sana, tofauti na miaka ya nyuma ambapo uzalishaji mwingi ulikuwa ukilenga kupatikana kwa bidhaa ghafi peke yake.*

*Aidha, kukua kwa uzalishaji huu unatokana na juhudi za serikali, mashirika binafsi na wadau, wahusika wenyewe kulenga zaidi kuzalisha kwa ajili ya kukuza na kuongeza pato, jambo lililosababisha kila mmoja kutafuta ubunifu wa kuzalisha bidhaa kamili na si kuuza bidhaa ghafi ambayo mara nyingi huleta hasara na kipato kidogo kwa wafugaji na wakulima.*

*Hata hivyo, pamoja na uzalishaji huu kuendelea kukua siku hata siku hasa katika sekta ya kilimo na ufugaji, bado wakulima na wafugaji pamoja na wajasiriamali wameshindwa kufikia lengo hili kwa asilimia kubwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kukosekana kwa elimu stahiki juu ya uzalishaji wa bidhaa husika, kukosekana kwa wataalamu wa kutosha kutoa elimu, vifaa duni, kupatikana kwa bidhaa ghafi zisizokidhi uzalishaji wa bidhaa kamili, kukosekana kwa pesa za kutosha kununua vifaa vinavyohitajika kuzalisha bidhaa husika n.k.*

*Kwa mantiki hii, wakulima na wafugaji hawana budi kuweka juhudi katika kupata kwanza elimu sahihi juu ya bidhaa fulani pindi wanapohitaji kuiongezea thamani na kupata bidhaa kamili, lakini pia kuhakikisha elimu hiyo wanaipata wapi na kwa wataalamu waliobobea kuhusu bidhaa hiyo na si kupata kwa watu wa mtaani tu ambao mwisho wa siku wanaishia kuzalisha bidhaa zisizokidhi soko.*

*Ni muhimu sana kwa wafugaji na wakulima kuhakikisha wanajua gharama sahihi kwa ajili ya kuanza kuzalisha bidhaa fulani. Hii itasaida wao kujipanga kifedha, na kuweza kumudu gharama zote za uzalishaji wa bidhaa husika ikiwa ni pamoja na manunuzi kwa ajili ya vifaa vya kutengenezea bidhaa hiyo.*

*Wadau wote wa kilimo na ufugaji yakiwepo mashirika binafsi na serikali haina budi kuweka mkazo na kujikita zaidi kwa wakulima na wafugaji wadogo katika kuwajengea uthubutu wa kuzalisha bidhaa kamili zilizoongezewa thamani, kuwapa elimu kamili, sahihi na kwa wakati sahihi ili waweze kuzalisha kwa ubora, kulenga soko na baadaye kujipatia kipato kinachoendana na kazi waliyoifanya.*

*Wakulima na wafugaji wanahitajika kutambua soko la bidhaa zao wanazotarajia kuzalisha. Pia kuwa wabunifu na kutokujikita wote katika kuzalisha bidhaa moja na kama ikitokea hivyo, kuwe na ladha mbalimbali au kuwe na utofauti ili kuweza kuweka ushindani kwenye soko.*

# Kilimo bora cha Chaya na umuhimu wake kwa jamii

*Chaya ni aina ya mbogamboga ambayo asili yake ni* Yucatan Peninsula *huko nchini Mexico na baadhi ya sehemu ya guatemala.*

***Flora Laanyuni***

Chaya ni sawa na spinachi na aina zingine za mbogamboga ya kijani, lakini yenyewe inakuwa kama mti wenye ujazo wa mita 3 (futi 10) na urefu wa mita 2 (futi 6.5) upana. Aidha, majani yake yana ukubwa wa usawa wa mkono wa mtu mzima.

Kwa karne kadhaa zilizopita, chaya ilikuwa chakula kikuu huko Mayans na ilijulikana kama chae, chatate au chaya mansa.



*Chaya aina ya Estrella ni nzuri kulima kwakuwa ina kiwango kingi cha lishe na mavuno mengi*

**Aina za Chaya**

Kuna aina nyingi za chaya lakini *Estrella* chaya (nyota) ndiyo yenye kiwango kikubwa cha lishe na majani mengi.

Kipindi cha ukame au baridi chaya inaweza kupoteza majani lakini yakarudi wakati wa mvua na jua.

**Uzalishaji wa chaya**

Moja kati ya chakula cha haraka na rahisi kuzalisha ni chaya. Chaya huzalishwa kirahisi sana kwa kutumia vipandikizi.

**Namna ya kuzalisha chaya**

Kata vipandikizi sehemu ya futi 8 hadi 12 ya tawi la chaya kisha panda kwa urefu wa futi 4 hadi 5 kwenye udongo ikiwa kwenye chungu au moja kwa moja kwenye udongo.

Hakikisha kuwa eneo lipo wazi na kuna jua na mwagilia kwa maji ya kutosha hadi utakapoona mizizi imeanza kujitokeza lakini usimwagilie kwa kipindi kirefu.

**Ukuaji wa chaya**

- Chaya hukua vizuri kwenye udongo wa kichanga na pia katika eneo lenye ukame.
- Mbolea si lazima katika ukuzaji wa chaya isipokuwa ikiwekwa mbolea na kumwagiliwa vizuri, chaya itachanua vizuri na kuweka majani ya kutosha.
- Chaya inaweza kulimwa sehemu za joto, sehemu za tropiki chini ya mita 600 (futi 2000) kutoka usawa wa bahari.
- Sehemu ya kupanda chaya ni lazima iwe imelindwa vizuri dhidi ya baridi na upepo wa baridi lakini pawe penye kupata jua la kutosha.
- Aidha, chaya hustahimili magonjwa ya aina mbalimbali na wadudu hivyo haisumbui katika udhibiti.

**Kwanini ulime na kula chaya?**

Majani ya chaya ni chanzo kikubwa cha madini ya chuma, protini, kalshiamu, Vitamini A, C, foliki, asidi na Vitamini B.

***Protini;*** inajenga misuli. Mlo mmoja tu wa chaya ni sawa na kiwango cha protini kinachopatikana kwenye yai.

***Madini ya chuma;*** Kwa afya ya damu na nguvu nyingi. Chaya ina kiasi kikubwa cha madini ya chuma mara mbili zaidi ya kiasi kinachopatikana kwenye spinachi.

***Kalshiamu;*** Kwa mifupa yenye nguvu, chaya ina kiasi kikubwa cha kalshiamu kuliko mboga zingine zote.

***Vitamini A;*** Inazuia upofu, inapunguza kiwango cha maambukizi ya magonjwa ya kuhara.

***Vitamini C, foliki asidi na Vitamini B;*** Vyote hivi ni muhimu sana kwa afya.

Kwa watoto wa miezi 6 hadi miaka 2, chaya halisi ni nzuri sana kwa kupata protini na vitamini hasahasa wakati ambapo wameachishwa kunyonya maziwa ya mama.

Supu ya chaya ni nzuri sana kwa watoto wa miaka 2 na kuendelea, na inaweza kutumika kama mlo ikichanganywa na vyakula vingine.

Mama anayenyonyesha ambae anakula chaya ana maziwa mengi na bora kwa ajili ya mtoto wake.

**Maandalizi ya chaya**

- Chaya ina asidi ya asili iliyoko kwenye chembechembe hai za majani. Mbogamboga nyingine kama kisamvu zina asidi lakini inaweza kuliwa kama ikipikwa.
- Kwa usalama wa kuondoa asidi, chemsha chaya kwa muda wa dakika 15 kwenye chombo ambacho siyo cha aluminiamu na kisha mwaga maji hayo.
- Kuchemsha majani makubwa kwa muda wa dakika 25 hadi 30 inaruhusiwa ili kuweza kuyafanya kuwa malaini.
- Kukatakata majani ya chaya kwa ajili ya kupika yanaweza kufanya kuwa rahisi kutafunwa na kumeng'enywa pia tumboni.

**>> Itaendelea Toleo Lijalo**

*Mkulima Mbunifu* ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa kila mwezi na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni moja wapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro.
Jarida hili linasambazwa kwa wakulima bila malipo.
*Mkulima Mbunifu* linafadhiliwa na Biovision - www.biovision.
**Wachapishaji** African Insect Science for Food and Health (icipe), S.L.P 30772 - 00100 Nairobi, KENYA, Simu +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org
**Mpangilio** Zenith Media Ltd
**Mhariri Msaidizi** Flora Laanyuni
**Mhariri** Ayubu S. Nnko
**Mhariri Mkuu** Venter Mwongera
**Anuani** *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction block)
S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
**Ujumbe Mfupi Pekee**: 0785 496 036, 0766 841 366
**Piga Simu** 0717 266 007, 0785 133 005
**Barua pepe** info@mkulimambunifu.org,
www.mkulimambunifu.org

# Umuhimu wa kufahamu vyanzo vya magonjwa ya mifugo



*Uzalishaji na upatikanaji wa mifugo yenye afya hutegemea utunzaji bora na wenye tija*

*Magonjwa mengi ya mifugo husambazwa na vijidudu ambao huingia kwenye mfumo wa damu na kusababisha homa na baadaye madhara makubwa.*

*Amani Msuya*

Magonjwa mengi ya mifugo husababishwa na vyanzo kutoka nje ya mwili wa mnyama mfano; mazingira machafu anayoishi mnyama, vitu vinavyopelekea vidonda (vitu vyenye ncha kali) ambavyo husababisha vidonda na baadaye vimelea vinaweza kukaa.

Pia mnyama anaweza kupata ugonjwa kutokana na hali za ndani ya mwili kama upungufu wa lishe, mfano; madini na magonjwa ya kurithi.

**Wadudu waenezi wa magonjwa ni kama vile;**

***Vimelea(bakteria)***

Mfano wa magonjwa yanayosababishwa na vimelea ni kama vile chambavu, *black quarter*, kimeta, kifua kikuu, *brucellosis*, ugonjwa wa kiwele, na ng'ombe dume kuvimba mapumbu.

***Virusi (virus)***

Mfano wa magonjwa yanayosababishwa na virusi ni kichaa cha mbwa (*rabies*), ugonjwa wa midomo na miguu (*foot and mouth disease*) nansotoka (*rinderpest*).

***Protozoa***

Magonjwa yanayosababishwa na protozoa ni kama ndigana baridi, ndigana kali, ndigana mkojo damu na ndigama maji moyo na nagana.

***Lishe duni***

Upungufu wa viinilishe katika chakula cha mifugo husababisha madhara katika mwili kama ifuatavyo;

- Husababisha majike kutopata joto mapema
- Ndama kuzaliwa na viungo visivyokomaa
- Upungufu wa uzalishaji wa maziwa
- Kiwango cha uzalishaji kushuka.

***Vidonda/michubuko***

Kupitia vidonda au michubuko, wadudu wasababishao magonjwa huingia mwilini mwa mnyama na kuleta madhara.

***Magonjwa ya kurithi***

Kama mmoja wa wazazi ana magonjwa au ugonjwa wa kurithi basi kuna uwezekano mkubwa wa mmoja wa ndama watakaozaliwa kurithi ugonjwa huo.

**Utunzaji bora wa afya ya mifugo**

***Uogeshaji***

Mifugo waogeshwe mara kwa mara ili kuepukana na magonjwa yaenezwayo na kupe pamoja na ndorobo. Uogeshaji unaweza kufanyika kwa kutumia pampu za mgongoni au kwa kuwatumbukiza katika josho lililotiwa dawa ya kuogesha.

***Kuwapa dawa za minyoo***

Mifugo wapatiwe dawa za minyoo mara kwa mara ili kuhakikisha ukuaji wao na utoaji wa maziwa uendelee vizuri. Mifugo wapewe dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu.

***Kuhasi***

Ndama dume wasiohitajika kwa ajili ya kuzalisha baadaye, wahasiwe kwa njia ya upasuaji au kwa kutumia koleo au badizo iwapo ndama ni wakubwa.

***Kuwapa ndama alama za utambulisho***

Ndama wapewe namba au alama za utambulisho mara wafikiapo miezi 6 tangu kuzaliwa na utambulisho huu unaweza kuwa wa chuma au wa plastiki chenye namba kwenye sikio.

***Kuondoa vishina au vichomozo vya pembe***

Ndama waondolewe pembe katika mwezi wa kwanza tangu kuzaliwa kabla vishina havijakomaa na kusababisha kushindwa kutoka kwa miezi ya mbeleni.

Tumia chuma cha moto kutoa vichomozo vyote vya pembe na hii husaidia ndama kukua katika mwonekano mzuri na kutokuwa na pembe zinazoweza kuumiza wenzake pindi ziwapo kubwa.

***Kuondoa kwato***

Kwato za ndama ziondolewe miezi mitatu ya mwanzo, ili kusaidia kupunguza kuondokana na magonjwa ambukizi ambayo husababishwa na kukatika kwa kwato zikiwa kubwa pindi awapo malishoni au akiwa katika banda lenye sakafu ya saruji.

***Kwa maelezo zaidi kuhusiana na ufugaji pamoja na makala hii wasiliana na mtaalamu kutoka SUA Bw. Agustino Chengula kwa simu namba 0767 605 098.***



*Namna ya kukata kwato*

# Namna nzuri ya uvunaji na uhifadhi wa samaki k

*Mavuno ya samaki hutoa picha halisi ya mafanikio katika ufugaji wa samaki endapo mfugaji atazingatia kanuni sahihi za uvunaji.*

**Musa Saidi**

Kama samaki watahudumiwa vizuri vizuri ndani ya miezi minne hadi sita samaki aina ya sato (Tilapia) wanaweza kuwa na uzito unaokadiriwa kuwa gramu 250 hadi 300 na kwa samaki aina ya kambale wanakuwa na uzito unaokadiriwa wa gramu 500 hadi 700.

Ukuaji huu unategemea samaki walipandwa bwawani wakiwa na ukubwa gani, idadi iliyopandwa na kiwango cha usimamizi wa mabwawa ambao unahusisha pia ubora wa maji.

**Maandalizi kwa ajili ya kuvuna**

- Hakikisha umeandaa soko la samaki utakao wavuna.
- Panga kuvuna samaki wako asubuhi na mapema au jioni sana.
- Usiweke mbolea wiki moja au mbili kabla ya kuvuna.
- Usiwape samaki chakula siku mbili kabla ya kuvuna.
- Andaa vifaa vyote vya kuvunia na jinsi ya kuwasafirisha samaki watakaovunwa.
- Andaa satu watakaovuna samaki
- Asubuhi na mapema punguza maji bwawani.

**Uvunaji**

- Uvunaji wa samaki bwawani unaweza kuwa na lengo la kuondoa samaki wote bwawani au kuvuna wachache tu.
- Uvunaji wa samaki unaohusisha kuwaondoa samaki wote bwawani unaweza kufanyika kwa kuondoa maji yote bwawani.
- Unapohitaji kuvuna samaki wachache ndani ya bwawa, unatakiwa kupunguza maji ili kurahisisha uvunaji. Baada ya kupunguza maji pitisha nyavu bwawani ili kupata idadi ya samaki unaowahitaji.

**Mambo ya kuzingatia unapovuna kwa kutumia nyavu**

- Uvunaji kwa njia ya nyavu ufanyike mapema asubuhi hali ya hewa ikiwa imetulia.
- Uvunaji uanzie sehemu ya bwawa yenye kina kirefu kuelekea sehemu ya bwawa yenye kina kifupi.
- Kazi ya uvunaji ifanyike kwa uangalifu mkubwa ili kupunguza utibuaji wa sehemu ya chini ya bwawa.
- Nyavu ilegezwe wakati wa uvunaji ili kuepusha samaki kurundikana sehemu moja hali inayoweza kuwasababishia msongo na hata majeraha.
- Kama inawezekana mwaga maji safi juu ya samaki wakati wanaponyanyuliwa kwa nyavu kutoka bwawani.
- Tumia chombo maalumu kuhamisha samaki kutoka kwenye nyavu na kuwaweka kwenye ndoo au chombo kingine kizuri ilichokichagua.


Samaki waliolishwa na kutunzwa vizuri huwa na mavuno yenye ub

Kwa samaki wanaouzwa wakiwa hai, wanapaswa kuvuliwa kwa uangalifu mkubwa.

***Mambo yafuatayo ni lazima yazingatiwe;***

- Samaki wahifadhiwe kwenye maji yaliyo safi muda wote.
- Samaki wahifadhiwe kwenye vyombo vyenye nafasi mara tu baada ya kuvunwa.
- Samaki wapelekwe sokoni haraka iwezekanavyo mara tu baada ya kuvunwa.
- Kama kuna uwezekano, samaki wawekewe vifaa vinavyoingiza hewa kwenye maji wanaposafirishwa kuelekea sokoni.

**Uhifadhi wa samaki**

Samaki anapoharibika ubora wake hupotea na kupungua, kuharibika kwa samaki huanza mara tu samaki anapokufa.

Uharibifu hupunguza kiwango cha viini lishe muhimu kwa afya ya mlaji.

Vilevile hushusha pato la mvuvi au mfanya biashara wa samaki au mfugaji jambo ambalo limekuwa likirudisha nyuma juhudi za kupambana na umasikini na utafutaji wa pato, hivyo ni vyema kujua njia bora za kuhifadhi samaki mara tu baada ya kuvuna.

***Kasi ya samaki kuharibika huchangiwa na;***

- Kuchelewa kutoa matumbo,magamba na matamvua.
- Kutoosha samaki vizuri kwa maji safi na salama.
- Kuweka samaki sehemu yenye joto (kwenye jua).
- Kutumia muda mrefu wakati wa

# wa lengo la kupata mavuno bora na kulenga soko



ora na yanayolenga soko

kutayarisha samaki.

- Kuchelewa kutoa samaki kwenye nyavu baada ya kunasa (kwa wavuvi wa maji ya asili).
- Kumjeruhi samaki wakati wa kuvuna au kuvua.

***Uharibifu wa samaki unaweza kupunguzwa kwa kuzingatia yafuatayo;***

- Kutoa matumbo, magamba na matamvua haraka bila kuchelewa.
- Kuosha samaki vizuri kwa kutumia maji safi na salama.
- Kuhifadhi samaki kwenye sehemu safi na yenye ubaridi.
- Kuhakikisha kuwa samaki hawakai mtegoni kwa muda mrefu mara baada ya kunasa.
- Epuka kujeruhi, kurusha hovyo na kukanyaga juu ya samaki.
- Hakikisha unawaweka katika hali ya usafi.

***Samaki akiharibika huwa na dalili zifuatazo;***

- Matamvua hubadilika kutoka rangi nyekundu kuwa ya kahawia.
- Samaki huwa laini akibonyezwa.
- Macho kwa ndani huonekana kama kuwa na ukungu.
- Pia wanaweza kutoa harufu mbafu mbaya.

**Njia za kuhifadhi samaki**

***Uhifadhi wa samaki kwa kuwakausha juani***

Hii njia hutumika kwa samaki wadogo zaidi kama dagaa.

***Uhifadhi samaki kwa kutumia joto la moshi***

Chagua samaki wenye ubora mzuri, wasafishe vizuri na toa magamba na matumbo yote kisha andaa maji yenye chumvi kiasi unachohitaji kulingana na wingi wa samaki kisha waweke samaki kwa muda ili chumvi ipate kukolea (chumvi ni muhimu ili kuleta ladha, kuzuia vijidudu na kusaidia samaki kukauka haraka).

Watoe samaki wote kutoka kwenye chumvi na wapange kwenye chaga za kukaushia kisha waache kwa muda ili maji yapungue kwenye samaki kisha washa moto kwenye tanuri jikoni na weka chaga zako juu ya tanuri na anza kukausha samaki wako kwa hatua tatu (joto la moshi, kupika na kukausha kwa joto).

Acha samaki wapoe na watoe kwenye *racks* zako, kisha wafungashe vizuri tayari kwa kuwapeleka sokoni.

***Uhifadhi samaki kwa kutumia chumvi***

- Chagua samaki walio bora na waandae kwa kuwaondoa matumbo, magamba na matamvua kisha waoshe vizuri kwa maji safi na salama.
- Kama samaki ni wakubwa basi wapasue.
- Andaa chombo kinachoruhusu au hata kisichoruhusu kutoa maji utakachotumia kwa kukaushia samaki.
- Anza kuweka tabaka la chumvi kwenye chombo ikifuatiwa na kuwalaza samaki juu ya tabaka hilo la chumvi. ***Angalizo***; samaki wasilaliane.
- Weka tabaka jingine la chumvi likifuatiwa na tabaka la samaki na endelea kufanya hivyo mpaka samaki waishe. ***Angalizo***; ni lazima tabaka la mwisho liwe ni chumvi.
- Funika kwa kitu kizito ili kusaidia kutoa maji kutoka kwenye mwili wa samaki.
- Waache samaki kwenye chumvi kwa muda wa siku 2 hadi 3.
- Watoe samaki kutoka kwenye chombo cha kukaushia na ondoa au pangusa mabaki yote ya chumvi.
- Waweke samaki kwenye kichanja na waanike kwenye jua hadi wakauke kabisa.
- Fungasha samaki wako vizuri tayari kwa kupeleka sokoni au kutumiwa.

***Uhifadhi wa samaki kwa kutumia barafu au kwa kuwagandisha kwenye jokofu***

Lengo la njia hii ni kupunguza joto la samaki hivyo vimelea viharibifu pamoja na kemikali hushindwa kufanya kazi. Unapotumia barafu, tumia uwiano wa 1:2 kati ya samaki na barafu.

***Kwa maelezo zaidi wasiliana na Bw. Musa S. Ngemetwa kwa simu 0718 986 328***

**>> Itaendelea Toleo Lijalo**



# Sindika Lusina kupata mbadala wa chakula cha kuku




*Majani mabichi na yenye rangi ya kijani ya mmea wa Lusina ndiyo yanayohitajika kwa ajili ya kusindika*

*Ulishaji wa kuku ni hatua moja muhimu na kubwa sana inayosumbua wafugaji wengi hasa wakati wa kiangazi ambapo vyakula vingi vya asili kama majani malaini ni vugumu sana kupatikana.*

***Ayubu Nnko***

Katika msimu wa kiangazi kunakuwa na uhaba mkubwa wa mboga za majani kwa ajili ya kulisha kuku jambo ambalo huwapa wafugaji wengi kujiingiza katika gharama kubwa za manunuzi ya vyakula vya kulishia kuku.

Kwa kupunguza na kuondoa kabisa adha hii, Lusina inaweza kutumika kuwalisha kuku msimu wa kiangazi kama mbadala wa mboga majani na kuku kupata vitamin zote zipatikanazo kwenye mbogamboga.

**Lusina ni nini**

Lusina ni mmea ambao unastawi maeneo mengi nchini Tanzania. Wakulima wengi wamezoea kulisha majani haya mbuzi na ng`ombe, bila kujua kuwa kumbe wanaweza kutumia majani haya ya lusina yaliyokaushwa na kuwalisha kuku ili wapate vitamin ambazo zinapatikana kwenye mbogamboga na kupunguza uhaba wa chakula wakati wa kiangazi.

**Mahitaji kwa ajili ya kuandaa**

Majani ya kutosha ya lusina, jamvi la kuanikia, kinu cha kutwangia au kusagia majani hayo, chekeche, na sehemu salama yenye kivuli ya kuanikia.

**Namna ya kuandaa/kusindika**

- Baada ya kuchuma majani ya kutosha ya lusina na kuyachambua kuondoa vitawi vidogovidogo anika majani hayo sehemu yenye kivuli ili ivirutubishe visipotee kwa njia ya jua.
- Acha sehemu hiyo kwa muda wa siku 5 hadi 7 kutegemeana na mazingira ya joto au baridi (kwenye joto lusina inakauka haraka).
- Baada ya hapo toa kivulini kisha anika juani masaaa mawili au matatu na hapo itakuwa tayari imekauka.
- Twanga kwenye kinu hadi ilainike vizuri kisha chekecha ili kupata unga.
- Hifadhi unga huo kwenye mifuko na tunza sehemu isiyo na ubichi kuzuia isiharibike kwa kuvunda.

**Matumizi**

- Katika msimu wa kiangazi au hata kama ni masika kama mboga za majani ni adimu kupata, wape kuku unga wa lusina kwa kuchanganya na maji yao ya kunywa.
- Tumia kijiko kimoja cha chakula kikubwa kwenye maji ya lita 3 kisha koroga vizuri na acha nusu saa.
- Maji hayo yatageuka kuwa ya kijani na wawekee kuku maji hayo wanywe.
- Kiasi cha kuwapa itategemea idadi ya kuku uliowafuga, na wape kuku mchanganyiko huo kila wiki mara 4 hadi 5.
- Mchanganyiko huo unawapa kuku wa rika zote. Kuku wanaotaga mayai kiini cha yai kitakuwa na rangi ya njano iliyokolea

Kuku watapata vitamini za kutosha kama vile ambavyo wangepewa mboga majani na njia hii imewasaidia wakulima wengi kuboresha mifugo yao na kukabiliana na upungufu wa vitamini.

**Uhifadhi wa unga wa lusina**

Unga wa lusina unaweza kuhifadhiwa kwa muda wa mwaka mmoja ukiwa na ubora huo huo.

Njia hii inaweza wasaidia wafugaji ambao maeneo yao mboga majani ni adimu.

**Muhimu**

Mchanganyiko huu unaweza kuongezwa na unga wa mifupa kikombe cha chai kwa lita mbili hadi tatu kwenye unga wa lusina, ili kuwaongezea madini ya chuma na chokaa kuku wako.

Madini ya chuma yanasaidia sana kuongeza chembechembe hai za damu, kuongeza madini joto katika kuhamilisha mifumo ya uzazi kwa kuku kutaga vizuri mayai.

Ukichanganya na unga wa mifupa unaweza kuwapa kuku kwa kuchanganya kwenye pumba lita 5 unga wa lusina lita mbili.

Ni matumaini yetu kuwa; wakulima wakifuatilia njia hii watapata mabadiliko makubwa sana katika shughuli zao za ufugaji kuku na kujiongezea kipato.

***Kwa maelezo zaidi unaweza kuwasilisana na mwezeshaji wa kilimo hai kutoka Mbeya Bw. Robert Haule (0757 751212).***

# Tambua faida na hasara ya mfumo utakaochagua kufugia kuku

*Mfugaji awaye yote, kabla ya kuanza mradi wa ufugaji wa kuku ni lazima kwanza akatambua ni mfumo gani ama ni njia gani atatumia katika ufugaji wake ili kuweza kujipanga kwa ajili ya mahitajia na gharama za mfumo husika.*

***Patrick Jonathan***

Mambo yanayomfanya mfugaji kuamua atumie njia fulani ya kufuga ni pamoja na uwezo wa kugharamia shughuli ya ufugaji wa kuku na ukubwa wa eneo alilonalo la kufugia.

Katika sehemu hii utajifunza mifumo au njia tatu za kufuga kuku ambazo ni:

**1. Kufuga katika mfumo huria**

Kuku huachwa wenyewe kujitafutia chakula na maji. Njia hii inatumika zaidi kufuga kuku wa kienyeji na ni mara chache sana mfugaji huwapatia kuku chakula cha ziada. Kwa ufugaji huu lazima kuwe na eneo kubwa la kutosha kuku kuzunguka na kutafuta chakula. Kuku hulala eneo lisilo rasmi kama vile jikoni, kwenye kiambata n.k

**Faida za mfumo huria**

- Ni njia rahisi ya kufuga.
- Gharama yake pia ni ndogo.
- Kuku wanapata mazoezi ya kutosha.
- Kuku wanapata chakula mchanganyiko ambacho kinafaa kiafya.

**Hasara zake**

- Kuku huwa hatarini kuibiwa au kudhurika na wanyama wakali na hali mbaya ya hewa.
- Ukuaji wa kuku ni hafifu, hufikia uzito wa kilo 1.2 baada ya mwaka.
- Huharibu mazingira kama kula na mimea ya bustanini mazao kama nafaka.
- Ni rahisi kuambukizwa magonjwa.

**2. Kufuga katika mfumo wa nusu huria**

Huu ni mtindo wa kufuga ambapo kuku wanakuwa na banda lililounganishwa na uzio kwa upande wa mbele. Hapa kuku wana uwezo kushinda ndani ya banda au nje ya banda wakiwa ndani ya uzio. Wakati wa mchana kuku huwa huru kushinda ndani ya banda hasa wanapotaka kutaga na wakati wa kuhatamia au wanaweza kukaa ndani ya uzio nje.



*Katika mfumo wa nusu huria mfugaji anaweza kuwatoa kuku nje ya banda nakuwalisha*

**Faida za kufuga nusu ndani na nusu nje**

- Kuku wanakuwa salama mbali na maadui mbali mbali.
- Utaweza kuwalisha kuku wako vizuri hivyo wataweza kuongeza uzalishaji wa mayai na wa nyama (kwa kukua haraka).
- Itakuwa rahisi kwako kudhibiti wadudu na vimelea vinavyoweza kuleta magonjwa kwa kuku wako.
- Ni rahisi kuwatenganisha kuku katika makundi tofauti na kuwahudumia ipasavyo.
- Ni rahisi kutambua kuku wagonjwa kuliko kufuga huria.
- Kuku watapata mwanga wa jua wa kutosha pamoja na hewa safi.Wakati wa jua kali watakuwa huru kuingia ndani ya banda na kukaa kivulini.
- Kuku hawatafanya huharibifu wa mazao yako shambani au bustanini na kwa majirani zako.
- Utapata urahisi wa kukusanya na kupeleka mbolea bustanini au shambani.

**Changamoto ya kufuga nusu ndani na nusu nje**

- Huna budi uwe na muda wa kutosha kwa ajili ya kuwahudumia kuku wako.
- Pia utahitaji kuwa na eneo kubwa kiasi la kufugia.
- Pia utaingia gharama ya ziada kidogo ya kutengeneza banda na wigo na kuwapatia uku chakula cha ziada.
- Hata hivyo gharama za muda huo na za vifaa vingine zitafidiwa na mapato ya ziada utakayopata kwa kufuga kwa njia hii.

**3. Kufuga katika mfumo wa ndani**

Njia nyingine ni kuwafuga kuku ndani tu. Katika njia hii, kuku hukaa ndani wakati wote. Njia hii ya ufugaji utumiwa zaidi na wafugaji wa kuku wa kisasa. Lakini yaweza kutumika hata kwa kuku wa asili hasa katika sehemu zenye ufinyu wa maeneo.

**Faida za kufuga ndani tu**

- Ni rahisi kutambua na kudhibiti magonjwa.
- Ni rahisi kudhibiti upotevu wa kuku, mayai na vifaranga.
- Ni rahisi kuwapatia chakula kulingana na mahitaji ya kila kundi.
- Ni rahisi kuwatambua na kuwaondoa kuku wasiozalisha katika kundi.

# Maoni kutoka kwa wasomaji wa jarida la MkM

*Jarida la Mkulima Mbunifu limeendelea kuchapisha mada mbalimbali zinazohusiana na kilimo na ufugaji hasa kwa kuzingatia misingi ya kilimo hai, jambo ambalo limeendelea kuonyesha matokea chanya kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.*

***MkM***



Picha: MkM

*Baadhi ya wanakikundi cha kahawa mkoani Kagera wakishirikishana elimu ya kilimo hai kutoka jarida la MkM*

Tumeona ni vyema kuchapisha baadhi ya pongezi na maoni yaliyotolewa na wadau na wasomaji wa jarida la Mkulima Mbunifu kupitia njia mbalimbali ikiwemo facebook, barua pepe (*email*), simu, barua na tovuti.

**Godson Kyara anasema;** Napenda chapisho hili la gugu karoti, ila naomba ndugu zangu tuwe makini kuzingatia athari za kiikolojia katika mazingira, kilimo, ufugaji na wanyama pori kwani kwa sasa wanaathiriwa sana na mimea vamizi (invasive alien plant species). Mpaka sasa taifa na hifadhi za taifa pia taasisi za kilimo na ufugaji huenda hazijui, zimepuuza au hazina uwezo wakuzuia na kudhibiti na hadi kufiki sasa mkoa wa Arusha umeathiriwa sana na gugu karoti. Tafadhali jamii kataeni mimea ya kigeni kwa kujua athari zake kimazingira katika eneo lako kabla hujapanda. Asanteni

**Felician Sway anasema;** Hongera sana Mkulima Mbunifu kwa kutukumbusha kuhusu nyanya za asili kwa sababu tumezoea tukipata vipya tunasahau vya zamani, Mungu akubariki sana.

**Peter Murage anasema;** Nchi yahitaji vijana kwani ndio tegemeo la kesho, hongera wana jarida wa Mkulima Mbunifu

**Rehema Sinda anasema;** Nimependa machapisho yenu, nitafanya mawasiliano kwa ***girl guides group*** ya mkoa wa Singida, na kikundi kingine nipate machapisho yenu kwa mafunzo.

**Gothel Pallangyo (gothelfpallangyo@gmail.com) anasema;** Nashukuru sana kwa elimu tuliyopata kutokana na gezeti la Mkulima mbunifu. Tumeweza kufaidika na mambo mbalimbali kama ifuatavyo;

1. Limewapa wakulima mwanga sana wa kufanya kilimo cha kibiashara na ufugaji bora.
2. Wanakikundi wameweza kusajili kikundi Brela na kujiunga na asasi za kifedha ili kukopesheka waweze kuitendea kazi elimu waliyoipata kutoka MkM.
3. Tunaomba elimu hii izidi kuwepo kwani tumepanua wigo na hadi sasa tunao wanakikundi wenginewaliokokikatitiambao tumeanza kuwapa elimu ya Mkulima Mbunifu.
4. Mpaka sasa tunao wanakikundi walioanza kufuga kuku, sungura, ng'ombe na mbuzi ila bado ni midogo ikitengemaa tutawajulisha Mwisho, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wote wanohusika na Mkulima Mbunifu.

**Maimuna Kanyamala (maimunakanyamala@hotmail.com) anasemma;** Ni kweli ni muda mrefu tunapokea na kufurahia jarida la *MkM*. Majarida haya ya kila Mwezi yamekuwa na mambo mazuri tafuatayo:

1. Linavutia kusoma kwa kuwa lina kurasa chache zenye picha za kuvutia na kuelimisha.
2. Nimefaidika na tumefaidika na elimu mnayoitoa kupitia jarida hili la MkM. Tumekuwa makini kwenye ufugaji na kilimo cha bustani. Tumeweza kusambaza elimu kwenye vikundi vingine. Pia tumewagawia wenzetu wa vijijini ambako elimu kama hii haipatikani kirahisi.
3. Kwa faida tunazozipata, huduma inafaa kuendelea sana
4. Ninapenda sana kushirikiana na wengine ili kujifunza zaidi. Kwa sasa najihusisha na kufuga kuku, sungura na kanga (nitatuma baadhi ya picha). Pia ninalima bustani ya mbogamboga.

Mimi naishi Buswelu, Mwanza. Plot 1794, Block C, North Buswelu. Simu zangu ni: 0767722229 na 0713722229. Ninawashukuru sana kwa elimu.